**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

Shule ya Sekondari ya Wasichana Ashira,
S.L.P. 345,
**MARANGU.**

Kumb. Na. ASH/S/24/55 30 Mei 2021

**Simu Na. 0767565445**
**Mkuu wa Shule 0754814403**
**Makamu Mku wa shule - 0768976221**
**Makamu Mkuu wa shule - 0754829481**
**Taaluma - 0754402138**
**- 0756236512**
**Malezi - 0754626631**

Ndugu_____________________________________________
______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA ASHIRA ILIYOKO WILAYA YA MOSHI VIJIJINI MKOA WA KILIMANJARO 2021/2022**

**1.** Ninafurahi kukuarifu na kukupongeza kwa kuchaguliwa kwako ____________________________________ Kujiunga na kidato cha TANO katika shule hii mwaka 2021/2022 tahasusi ya _______________. Shule ya Sekondari ya Wasichana Ashira ipo umbali wa km. 45.5 kutoka Stendi kuu ya mabasi ya Moshi Mjini. Kutoka Moshi Mjini hadi Marangu Mtoni utapanda mabasi yaendayo Mwika au Kilema kwa nauli ya shilingi 1,500/= (elfu moja na mia tano tu). Shuka Marangu Mtoni. Chukua taxi kwa nauli ya shilingi 3,000/= (elfu tatu tu) hadi shuleni ambapo ni km 1.5 tu.

Muhula wa masomo unaanza tarehe _________Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe_________ Tafadhali njoo na "**Hati ya Matokeo halisi**" **(Original Result Slip).**

**2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:-**

**A. SARE YA SHULE**

(i) Sare ya Shule hii ni sketi mbili ndefu na Bolero mbili aina ya Takroni Dark Blue. Blauzi / shati mbili rangi nyeupe tetron ya mikono mifupi, blanketi moja.
(ii) Sweta moja rangi ya Dark Blue yenye shingo V isiyo na vifungo.
(iii) Viatu vyeusi vya ngozi jozi mbili vya kufunga kwa kamba (gidamu) vinavyofunika miguu na visiwe na visigino (flat sole).
(iv) Soksi nyeupe ndefu jozi mbili zisizo na urembo (Royal-Free size).
(v) Polineck nyeupe ya mikono mirefu kwa ajili ya kujikinga na baridi.

(vi Tracksuit rangi ya Dark Blue aina ya Adidas au Puma yenye mistari mieupe kwenye mikono na pembeni mwa suruali isiwe na kofia, kwa ajili ya kuvaa wakati wa usiku (evening preparation) kwa ajili ya baridi na kuzuia kuumwa na mbu.

(vii) Aje na chandarua nyeupe kwa ajili ya kujikinga na mbu. Nguo ya kazi (working dress) gauni aina ya Takron Dark Blue. Kitambaa kimeambatanishwa. Aje na nguo ya kulala usiku (Night dress rangi aina yoyote.

(viii) Bukta ya rangi ya Dark Blue, T-shirt ya blue inayofanana na sketi, raba nyeusi kwa ajili ya michezo.

(ix) Wanafunzi wa Kiislamu waje na Hijabu mbili nyeupe na moja ya rangi Dark blue ambayo inafanana na rangi ya sketi. Hijabu zote ziwe na urefu na upana wa wastani.

(x) Nguo za nyumbani hazihitajiki. Tafadhali kwani muda mwingi atakuwa kwenye sare ya Shule na wakati wa kazi atavaa nguo za kazi

**MUHIMU:**
Sare ya Shule inayotakiwa ni kama michoro iliyoambatishwa inavyoonesha.

**B. ADA NA MICHANGO YA SHULE**

(i) Ada ya Shule kwa mwaka ni shilingi elfu sabini (70,000/=) kwa mwanafunzi wa bweni. Ada hii inaweza kulipwa kwa awamu mbili ambayo ni kiasi cha shilingi elfu thelathini na tano (35,000/=) kwa muhula.

(ii) Michango inayotakiwa na kila mzazi/mlezi

**MCHANGANUO:**

| | | |
|---|---|---|
| (a) | Ada (karo) kwa mwaka ............ | 70,000/= |
| (b) | Ukarabati wa samani............ | 15,000/= |
| (c) | Kukodi godoro kwa mwaka............ | 10,000/= |
| (d) | Picha na kitambulisho............ | 5,000/= |
| (e) | Taaluma kwa mwaka ............ | 20,000/= |
| (f) | Wapishi kwa mwaka............ | 20,000/= |
| (g) | Huduma na matibabu binafsi kwa mwaka............ | 10,000/= |
| (h) | Ulinzi kwa mwaka............ | 20,000/= |
| (i) | Tahadhari............ | 5,000/= |
| | **Jumla ya fedha zote ni shilingi (Laki moja na sabini na tano tu )** | **175,000/=** |

Fedha zote zilipwe katika Benki ya NMB Tawi la Nelson Mandela Moshi
JINA LA AKAUNTI **Ashira Girl's Secondary School Account number 40301200159** Tafadhali andika jina la Mwanafunzi, kidato na mchepuo. Fedha zote zinaweza kulipwa katika Benki ya NMB Tawi lolote lililo karibu kwa jina la akaunti ya Shule iliyotajwa hapo juu. Tafadhali leta Bank Pay in Slip halisi kwa ajili ya uthibitisho wa malipo

**MUHIMU:**
Fedha taslimu hazitapokelewa Shuleni kwa sababu za kiusalama. Kabidhi "Bank-Pay-in slip kwa Mwalimu atakayekupokea.

## C.VIFAA VYA USAFI WA MAZINGIRA:

**Unatakiwa uje na vifaa vifuatavyo kwa ajili ya usafi wa mazingira ya Shule.**

**Wanafunzi wote wa E.G.M.** - Mfagio mmoja mfupi wa chelewa na mmoja wa ukindu kwa ajili ya kufagia nje, hard broom, kijembe kidogo chenye pande mbili za rato na chuma.

**Wanafunzi wote wa H.G.L** _ Waje na Drying Mopper (Chombo cha kukausha maji) mfagio mrefu wa chelewa wa kufagia nje, hard broom, reki na ndoo ya plastiki.

**Wanafunzi wote wa H.G.E.** _ Waje na drying Mopp (Chombo cha kukausha maji) "Soft Broom", "Toilet Brush", panga na ndoo ya plastiki.

Wanafunzi wote wa C.B.G. _ Walete jembe na mpini, Hard Broom, Soft Broom na ndoo ya plastiki.

**Wanafunzi wa H.K.L.** – Mfagio mrefu wa chelewa wa kufagia nje na panga lililonolewa Fyekeo, na ndoo ya plastiki.

Kabidhi vifaa hivi kwa mwalimu atakayekupokea. Tafadhali mzazi/mlezi binti yako alete vifaa husika na siyo fedha taslimu.

## D. VIFAA BINAFSI

Mwanafunzi aje na vifaa vifuatavyo kwa mahitaji yake akiwepo shuleni:-

(j) Sanduku la bati saizi ya kati (medium size).

(ii) Shuka tatu (03) rangi ya pinki moja itatumika kama "Bed Cover" na Blanketi moja.

(iii) Mto mmoja(01) na foronya mbili (02) rangi ya pinki na ndoo ya plastiki.

(iv ) Vyombo vya kulia chakula- kijiko, bakuli, kikombe na sahani. Vyote vinapatikana katika duka la shule.

(v ) Malapa, dawa ya meno, mswaki, barakoa zisizopungua tano za kitambaa, vitakasa mikono na kalamu pia vinapatikana katika duka la shule Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi (cm.1) mm10 na kucha ziwe fupi bila rangi.

## VIFAA VYA MASOMO:

(i) Wanafunzi wa michepuo ya H.G.E., C.B.G na E.G.M. waje na Scientific Calculator na stapler. Vilevile wanafunzi wa CBG walete Dissecting kit.

(ii) Wanafunzi wote wa H.G.L. na H.K.L. waje na:-

"Oxford Advanced Learner's Dictionary- Current English by A.S. Hornby.

Advanced Level English Language Paper 1 & 2 by Nicholaus Ashel.

The Beautyful Ones Are Not YET Born by Ayi Kwei Armah.

(iii) Kwa **HKL** pia walete vitabu vifuatavyo:-
- Morani kimeandikwa na Emmanuel Mbogo
- Mfadhili kimeandikwa na Hussen Tour.

**USHARI**- Kimbunga – Haji Gora
Mapenzi Bora – Shaban Robert
**RIWAYA** - Kufikirika – Shabaan Robert
-Vuta N"kuvute – Shafi Adam Shafi

**TAMTHILIYA** – Nguzo Mama – Penina Muhando

(iv) Kila mwanafunzi alete daftari kubwa (counter books) zisizopungua 10, kalamu za wino, risasi, rula n.k.(Pia vinapatikana katika duka la shule).
(v) Wanafunzi wote walete "Ream moja ya karatasi (Duplicating paper A4) aina ya NOPA au JACANA. Utaikabidhi kwa mwalimu atakayekupokea.
(vi) Jitahidi kuleta vitabu vya masomo yako angalau viwili (02)

## FEDHA ZA MATUMIZI (POCKET MONEY)

Mzazi/Mlezi umpe mwanao fedha za matumizi kiasi cha kuridhisha kulingana na uwezo wa mzazi/mlezi. Ushauri epuka kumpa mwanao fedha nyingi mno kwani zinaweza kuwa kichocheo cha wizi hapa shuleni pia mwanao kuwa na tabia ya majivuno ambayo siyo nzuri.

**MUHIMU:**

Ni wajibu wa kila mwanafunzi kuhudhuria vipindi vya DINI yake husika akiwapo shuleni. Hairuhusiwi kabisa mwanafunzi kubadilisha DINI/DHEHEBU akiwepo shuleni bila idhini ya wazazi kwa maandishi.

Vitabu vya dini kwa ajili ya sala na vipindi vya dini hapa shuleni ni kama inavyoonesha:-

(i) Waislamu - Njoo na Quran Tukufu.

(ii) Wakatoliki - Njoo na Misale ya Waumini, Biblia na Rozari.

(iii) Waprotestant chini ya CCT – walete Biblia na Mwimbieni bwana/Tumwabudu Mungu.

Madhehebu mengine ya Kikristo njoo na Biblia na vitabu vya nyimbo kwa mujibu wa imani yako. Mfano Wasabato, Pentekoste n.k.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA MOSHI

SHULE YA SEKONDARI ASHIRA

## 3. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

### A. SHERIA:

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu namba 25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti Shuleni.

(a)Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

(b)Mahudhurio mazuri katika shughuli za ndani na nje ya darasa ni muhimu.

(c )Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni (preparation).

(d)Kuwahi katika kila shughuli za Shule na nyingine utakazopewa ambazo ni halali.

(e)Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika Shule hii.

(f)Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya Shule.

(g)Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.

(h)Kuzingatia ratiba ya Shule wakati wote.

(i)Hairuhusiwi kuja na aina yoyote ya vyakula Shuleni. Tafadhali Wazazi/Walezi fedha za ada , michango, na fedha za matumizi (Pocket money) ziwekwe kwenye Akaunti husika. Njia za kutuma fedha kama M-Pesa isitumike. Hii ni kwa ajili ya usalama.

## B. MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA UFUKUZWE SHULE:

1. Wizi.
2. Kutokuhudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro.
3. Uasherati na uhusiano wa jinsia moja.
4. Ubakaji.
5. Ulevi wa pombe, matumizi ya madawa ya kulevya na uvutaji wa sigara.
6. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au na mtu yeyote.
7. Kugoma au kuhamasisha mgomo.
8. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzako na jamii kwa ujumla.
9. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
10. Kudharau bendera ya taifa.
11. Kuoa au kuolewa.
12. Kusababisha, kupata mimba, kuharibu mimba au kutoa mimba ndani na nje ya shule.
13. Kukataa adhabu kwa makusudi
14. Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi (viganjani) au vifaa vingine vya umeme kama heater radio katika mazingira ya shule.
15. Ni marufuku kuvaa bangili, hereni, mikufu, kupaka rangi za kucha, lipstick, kupaka wanja na kutinda nyusi.
16. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi, walimu, walezi na jamii kwa ujumla.
17. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
18. Kufuga ndevu.
19. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
20. Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua kama kunywa sumu nk.

## 4. WAZAZI/WALEZI NA WAGENI:

Wazazi/Walezi na wageni watawaona wanafunzi siku ya kikao cha wazazi/walezi na siku za mahafali. Mzazi usishtushwe na barua za mwanao au kupata taarifa isiyo rasmi. Iwapo lipo tatizo uongozi wa Shule utakujulisha Ikiwa kuna shida muhimu mfano msiba wa baba/mama au mlezi kisheria taarifa iletwe kwa uongozi wa Shule kuwepo na uthibitisho wa kifo mfano barua ya Mwenyekiti wa Kijiji/Mtaa. Hii ni kudhibiti ulaghai wa baadhi ya watu wachache wanaotumia mianya hiyo kuwapotezea wanafunzi muda wa kusoma
Wazazi/Walezi wanaruhusiwa kuwaona wanafunzi siku ya Kikao cha wazazi/walezi ambacho hufanyika mara moja kwa mwaka. Tarehe kamili utajulishwa na siku ya Mahafali ya kidato cha Sita ambapo Wazazi/Walezi wanakaribishwa.

## 5. RIPOTI KUHUSU MAENDELEO YA MASOMO, TABIA NA MWENENDO WA MWANAFUNZI SHULENI:

Ripoti ya Shule kuhusu maendeleo ya mwanafunzi kimasomo, tabia na kazi za mikono itapelekwa kwa Mzazi/Mlezi kila baada ya kumaliza muhula. Mwanafunzi atatakiwa kutoa stampu na bahasha yenye anuani sahihi ya Mzazi/Mlezi kutuwezesha kutuma ripoti hiyo.

## 6. MAMBO MENGINE MUHIMU YA KUZINGATIA FOMU ZIMEAMABATISHWA:-

1. Medical Examination Form ambayo itajazwa na mganga mkuu hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mwalimu atakayekupokea mara utakaporipoti shuleni
2. Fomu ya maelekezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki migomo, fujo na makosa ya jinai.
3. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni kulipa ada, michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na Shule.
4. Fomu ya makubaliano.
5. Alete picha (Passport size) za Wazazi/Walezi.
   Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII NA UTAYARI WA KUJIFUNZA NA KUSHRIKI KATIKA SHUGHULI HALALI ZA KUIMARISHA NA KUPANUA MAARIFA NA UJUZI WAKO KWA MAISHA YAKO NA TAIFA KWA UJUMLA**

**E.J. ABDALLAH**
**MKUU WA SHULE**
HEADMISTRESS
ASHIRA GIRLS' SECONDARY SCHOOL
MOSHI

AINA YA KITAMBAA CHA SKETI, BOLERO NA NGUO YA KAZI NI DARK BLUU.

RANGI YA KITAMBAA CHA SARE YA SHULE INAFANANA NA SURUALI ZA TRAFIC POLICE WANAWAKE.

A. SKETI. Zipu iwe ya mbeleni siyo ya nyuma. Marinda ya Sketi yaelekee upande mmoja. Marinda yaanzie 12 na yasizidi 16.

A.



Sketi iwe ndefu inayofikia vifundo vya miguu.

B. NGUO YA KAZI (WORKING DRESS

Baby Collor

Mshono ni Solo isiwe pana sana.



Gauni liwe refu lenye mikanda. Rangi ya gauni inafana na rangi ya Sketi.

D


SWETA

RANGI DARK BLUU

C BOLERO



Bolero isiwe na vifungo wala zipu.



"SHAMI" – TAHASUSI YA EGM WALETE KIFAA KILICHOONESHWA.

**FOMU A**

**HATI YA MAKUBALIANO**

**ANWANI**

Mkuu wa Shule,
Shule ya Sekondari Ashira,
S.L.P. 345,
**MARANGU.**

**YAH: <u>KUKUBALI KUFUATA SHERIA NA MASHARTI YA SHULE</u>**

Mimi______________________________________________________________________
Nakubali nafasi ya Kidato cha____________________niliyopewa katika shule yako. Nayakubali masharti na kuwa nitatii sheria za shule hizo zilizoko na zile zitakazotolewa kwa muda wote wa masomo yangu. Naahidi kuwa nitawaheshimu na kuwatii walimu wote wa shule na wafanyakazi kama Walezi wangu. Naahidi kuwa nitatii wale wote watakaoteuliwa au kuchaguliwa kuwa viongozi wangu kwa mujibu wa sheria.

Naahidi kuwa nitakuwa mwanafunzi mwaminifu. Naahidi pia kuwa nitajielimisha kwa nguvu zangu na akili zangu zote kwa manufaa yangu binafsi na Taifa langu.

Natambua kuwa nikikiuka ahadi hizi nitapoteza nafasi yangu hapa shule.

JINA LA MWANAFUNZI_______________________________________________
SAHIHI_________________________________________________________

JINA LA MZAZI/MLEZI______________________________
SAHIHI_______________________________________

Anwani ya Mzazi/Mlezi_________________________________
_________________________________
Simu Na./E. Mail____________________

Namba ya kuandikishwa______________________________Tarehe__________________
Darasa ulilopangwa_________________________________ Bweni__________________
Jina la Mwalimu mlezi_________________________________ Sahihi__________________

**FOMU B**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ELIMU,SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI**

Shule ya Sekondari ya wasichana Ashira,
S.L.P. 345,
**MARANGU.**

Kumb. Na. ASH/A/24/55

30 Mei, 2021

**FOMU YA MAPOKEZI SHULENI – MAELEZO KUHUSU MWANAFUNZI**

Sehemu A: Ijazwe na mwanafunzi
(1)Jina la mwanafunzi (majina matatu)______________________________
______________________________
(2) Taifa______________________________
(3)Tarehe ya kuzaliwa______________________________
(4) Dini______________________________
(5) Shule anayotoka______________________________
Tarehe ya kutoka Shule______________________________
______________________________

**SEHEMU B: (IJAZWE NA MZAZI/MLEZI)**

(1) Jina la mzazi/mlezi(majina matatu)
______________________________
(2) Mahali unapoishi Kata____________________Kijiji____________
(3) Anuani ya mzazi/mlezi____________________Namba ya simu__________
(4) Kazi ya mzazi/mlezi____________________Mahali anapofanya kazi na anwani
______________________________

Ndugu wawili wa karibu (unaowaelewa badala ya mzazi/mlezi):-
(a) Jina______________________________
Anwani______________________________
Simu namba______________________________
Uhusiano wake na mzazi/mlezi______________________________
(b)Jina______________________________
Anwani______________________________
Simu namba______________________________
Uhusiano wake na mzazi/mlezi______________________________
Jina la mzazi/mlezi______________________________
Tarehe______________________________
Sahihi______________________________

**FOMU C**

Shule ya Sekondari Ashira,
S.L.P. 345,
**MARANGU.**

30 Mei, 2021.

**AHADI/MKATABA WA MWANAFUNZI**

Mimi mwanafunzi (majina matatu) ____________________________________________

____________________________________________________________________________
Ninaahidi kufuata taratibu na sheria zote za shule ikiwa ni pamoja na kutokushiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.

Saini________________________________________Tarehe__________________________

**AHADI YA MZAZI/MLEZI**

Mimi mzaz/mlezi mwanafunzi____________________________________________________
Kidato cha tano__________________________________mwaka_______________________
Ninakiri kukubaliana na sheria, kanuni, kulipa ada, michango ya shule na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule kwa kipindi chote mwanangu atakachokuwa katika shule ya Ashira Sekondari.

Jina la mzazi/mlezi______________________________________Saini_________________

Tarehe_________________________________

**FOMU D**

**PRESIDENT'S OFFICE**
**REGIONAL AEMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**
**MOSHI DISTRICT COUNCIL**
**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

Ashira Girls Secondary School,
P.O. Box 345,
**MARANGU.**

30 Mei, 2021.

The Medical Officer
**GOVERNMENT HOSPITAL.**

Name of pupil______________________________________________

Please examine the above named pupils and arrange any necessary treatment so that Certificate can be signed and the pupil can return it in time for the beginning of next term.

**MEDICAL CERTIFICATE (To be filled by Medical Officer).**

I have Examined the above named with regard to
REMARKS:-
Skin______________________________
Eyes______________________________
Ears______________________________
Tooth/teeth______________________________
Blood______________________________
Pressure______________________________
Abdomen______________________________
Urine______________________________
Stool______________________________
HB Hemoglobin______________________________
Any disabilities ______________________________
TB ______________________________

And consider that

(1) The pupil is in good health free from infections disease, worms, bilharzias and is fit to return to school.
(2) She is now fit to return to school after being treated for

______________________________________________
______________________________________________
______________________________________________

Name and signature of Medical Officer______________________________
Date______________________________